

MAKAO MAKUU

Ghorofa ya 4, Jengo la LAPF, Barabara ya Makole
S.L.P. 2857, Dodoma, Tanzania

Simu: +255-26 2329002-3; Nukushi: +255-26 2329005

Barua pepe: info@ewura.go.tz Tovuti: <http://www.ewura.go.tz>

TANGAZO KWA UMMA

MWITO WA MAONI YA WADAU KUHUSU MAOMBI YA MAREKEBISHO YA BEI ZA MAJI YA JUMLA KUTOKA MAMLAKA YA MAJI YA KAHAMA/SHINYANGA (KASHWASA) KWA MWAKA 2018/19 – 2020/21

Maombi ya Mabadiliko ya Bei Na. TR-W-18-006

Mnamo tarehe 16 Juni 2018 Mamlaka ya Udhubiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), ilipokea maombi yaliyokamilika kutoka Mamlaka ya Maji Safi ya Kahama/Shinyanga (KASHWASA) ya kutaka kurekebisha bei za huduma zake za majisafi kwa mwaka 2018/19 hadi 2020/21. Jedwali namba 1 linaonesha mchanganuo wa bei za sasa na zinazopendekezwa.

Jedwali Na 1: Bei za Sasa na Zinazopendekezwa kwa Maji ya Jumla (Shilingi kwa Unit)

Kundi la Wateja	Bei za Sasa	Mabadiliko kwa asilimia	Bei Zinazopendekezwa				
	2017/18		2018/19	Mabadiliko kwa asilimia	2019/20	Mabadiliko kwa asilimia	2020/21
Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira	580	46%	848	14%	970	11%	1,075
Kamati za Maji za Vijiji	435	46%	636	15%	730	11%	810
Uchimbaji wa Madini	1,000	25%	1,250	16%	1,450	9%	1,580

Mamlaka ya Majisafi ya KASHWASA imeeleza kuwa sababu ya msingi ya kuomba marekebisho ya bei ni ili kuweza kumudu gharama zote kama ilivyoelekezwa katika

Sera ya Maji ya 2002. Pia, KASHWASA imeeleza kuwa kutokana na makubaliano (MoU) kati yake na Wizara ya Maji na Umwagiliaji, KASHWASA inatakiwa kulipia ankara ya umeme kwa ajili ya uzalishaji wa maji kwa asilimia 100 kuanzia mwezi Julai 2018. Kwa sasa, Serikali kupitia Wizara inatoa ruzuku ya asilimia 20 kwa kila mwezi kwa ajili ya ankara ya umeme ambayo kwa kiasi kikubwa hailipwi kwa wakati. Hii inasababisha kukatiwa huduma ya umeme na kuleta madhara kwa utoaji huduma kwa wateja. Kwa hiyo, bei zinazopendekezwa zitaaidia KASHWASA kulipia ankara ya umeme bila kutegemea ruzuku kwa Serikali na kwa sababu hiyo kuhakikishia upatikanaji wa huduma kwa wateja.

Kwa mujibu wa kifungu Na. 19 (2) (b) cha Sheria Na. 414, kutakuwa na Mkutano wa Taftishi siku ya **Alhamisi, tarehe 9 Agosti 2018 katika Ukumbi wa mikutano wa TFS NAFRAC** uliopo Manispaa ya Shinyanga kuanzia saa **4:00 asubuhi**. Lengo la mkutano huo ni kwa ajili ya kupata maoni ya wadau ikiwa ni pamoja na Baraza la Ushauri la Serikali na Baraza la Ushauri la watumia Huduma zinazodhibitiwa na EWURA, wateja wa KASHWASA na wananchi wote kwa ujumla kuhusu uhalali wa bei zinazopendekezwa.

Wadau wanaopenda kutoa maoni kwa maandishi wanaombwa kufanya hivyo kwa kutuma maoni yao kwa Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa EWURA kwa anuani iliyoonesha hapo juu **ifikapo tarehe 14 Agosti 2018**. Maelezo zaidi yanaweza kupatikana katika ofisi za **EWURA MAKAO MAKUU, GHOROFA YA NNE, JENGO LA LAPF; BARABARA YA MAKOLE, DODOMA** au **OFISI ZA MAMLAKA YA MAJISAFI YA KASHWASA SHINYANGA**.

Imetolewa na:

Kaimu Mkurugenzi Mkuu

23 Julai 2018

